JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

# TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2022







MEI 2023

**Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2022**
**Imetayarishwa na mamlaka**
**ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.**

**S.L.P 80327,**
**8 Barabara ya Kivukoni,**
**11486 Dar es Salaam**
**Barua pepe: cg@dcea.go.tz**
**Tovuti: www.dcea.go.tz**
**Instagram: @dceatanzania**
**Twitter: @dceatanzania**
**Facebook: dcea_tz**
**YouTube: DCEATV**
**Simu ya bure: 119**

**ISBN:978-9912-9896-3-4**

**Imetayarishwa kwa mujibu wa sheria ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na.5 ya mwaka 2015**

## YALIYOMO

YALIYOMO ........ ii
ORODHA YA MAJEDWALI ........ v
ORODHA YA VIELELEZO ........ vi
MAELEZO YA WAZIRI ........ vii
DIBAJI ........ vii
FAHARASA ........ 1

**SURA YA KWANZA ........ 1**

**HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani ........ 1
1.2.1 Bangi ........ 1
1.2.1.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari Zake ........ 2
1.2.2 Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni ........ 2
1.2.3 Cocaine ........ 2
1.2.4 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya ........ 3
1.2.5 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substance s - NPS) ........ 3
1.2.6 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetamine Type Stimulants-ATS) ........ 4
1.3 Dawa za Kulevya na Jinsia ........ 5
1.4 Dawa za Kulevya na UVIKO 19 ........ 6

**SURA YA PILI ........ 7**

**MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI ........ 7**

2.1 Utangulizi ........ 7
2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction) ........ 7
2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kule vya (Demand Reduction) ........ 7
2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) ........ 7
2.5 Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ........ 8

**SURA YA TATU ........ 9**

**KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA ........ 9**

3.1 Utangulizi ........ 9
3.2 Udhibiti wa Upatikanaji wa Dawa za Kulevya ........ 9
3.3 Dawa Nyingine za Kulevya ........ 14
3.4 Watuhumiwa wa dawa za kulevya waliokamatwa nje ya nchi ........ 14
3.5 Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals) ........ 14
3.6 Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Kemikali Bashirifu ........ 15

3.7 Udhibiti wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya ....................16
3.8 Uchunguzi wa Kimaabara wa Dawa za Kulevya ....................16
3.9 Kaguzi zilizofanyika katika Kudhibiti Dawa Tiba zenye asili ya Kulevya....................17
3.10 Maboresho ya Sheria ....................17
3.11 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya ....................18
3.12 Kesi za Dawa za Kulevya ....................19

**SURA YA NNE....................20**

**KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA....................20**
4.1 Utangulizi ....................20
4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya ....................20
4.2.1 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya....................20
4.3 Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya ....................21
4.3.1 Kiafya ....................21
4.3.2 Kijamii ....................22
4.3.3 Kiuchumi ....................22
4.3.4 Kimazingira ....................22
4.3.5 Unyanyapaa ....................23
4.4 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya ....................23
4.4.1 Kazi za Uelimishaji zilizofanywa na Mamlaka....................23
4.4.2 Uelimishaji uliofanywa na Asasi za Kiraia....................26

**SURA YA TANO....................31**

**KUPUNGUZA MADHARA YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA ....................31**
5.1 Utangulizi ....................31
5.2 Huduma za Upunguzaji Madhra kwa Waraibu ....................31
5.2.1 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya Katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini ....................31
5.5.2 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Wara ibu wa Dawa za Kulevya ....................32
5.2.3 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)....................33
5.3 Huduma ya Upunguzaji wa Madhara ya Uchangiaji wa Sindano kwa Wajidunga....................36
5.4 Umuhimu wa Huduma za Upunguzaji madhara kwa Waraibu ....................37
5.5 Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka katika mwaka 2022....................37

**SURA YA SITA....................39**

**USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA....................39**
6.1 Utangulizi ....................39
6.2 Ushirikiano wa Kitaifa....................39

6.3 Ushirikiano wa Kimataifa ............................................................ 39
6.4 Ushirikiano wa Kikanda ............................................................ 41

**SURA YA SABA ............................................................ 42**

**CHANGAMOTO NA MIKAKATI ............................................................ 42**
7.1 Utangulizi ............................................................ 42
7.2 Changamoto ............................................................ 42
7.3 Mikakati ............................................................ 42

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kwa muongo mmoja (mwaka 2013 -2022) ... 9
Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2013-2022 ... 10
Jedwali Na. 3.3: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Katika muongo mmoja (Mwaka 2013-2022) ... 11
Jedwali Na. 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa katika muongo mmoja (Mwaka 2013-2022) ... 13
Jedwali Na. 3.5: Kiasi cha methamphetamine na mescaline kilichokamatwa mwaka 2021 - 2022 ... 14
Jedwali Na. 3.6: Mwenendo wa Uingizaji wa Kemikali Bashirifu Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 ... 15
Jedwali Na. 3.7: Kiasi cha Kemikali Bashirifu kilichozuiliwa kuingia nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 ... 16
Jedwali Na. 3.8: Sampuli za Dawa za Kulevya zilizofanyiwa Uchunguzi Mwaka 2022 ... 17
Jedwali Na. 3.9: Jumla ya kesi zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini ... 19
Jedwali Na. 4.1: Asasi zilizotoa Elimu ya Dawa za Kulevya Mwaka 2022 ... 26
Jedwali Na. 5.1: Idadi ya Waraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini Mwaka 2022 ... 32
Jedwali Na. 5.2: Idadi ya Waraibu waliosajiliwa kwenye Huduma za MAT hadi kufikia Desemba 2022 ... 33
Jedwali Na.5.3: Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu Mwaka 2022 ... 34
Jedwali Na. 5.4: Idadi ya Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu kuanzia mwaka 2019 hadi Mwaka 2022 ... 36
Jedwali Na. 5.5: Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka mwaka 2022 ... 38

## ORODHA YA VIELELEZO


| | | |
|---|---|---|
| Kielelezo Na. 1.1 | Watumiaji wa Dawa za Kulevya Duniani mwaka 2020 | 5 |
| Kielelezo Na. 3.1: | Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2013-2022 | 10 |
| Kielelezo Na. 3.2: | Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa kwa Kujihusisha na Bangi na Mirungi Nchini Kati ya Mwaka 2011 – 2020 | 11 |
| Kielelezo Na. 3.3: | Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2013-2022 | 12 |
| Kielelezo Na. 3.4: | Shehena ya kilo 859.36 za dawa za kulevya zikijumuisha kilo 504.36 za heroin na kilo 355 za methamphetamine zilizokamatwa Bahari ya Hindi eneo la Kilwa Masoko, mkoani Lindi | 13 |
| Kielelezo Na. 3.5: | Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa kati ya Mwaka 2013 - 2022 | 13 |
| Kielelezo Na. 3.6: | Zoezi la uteketezaji wa dawa za kulevya lililofanyika katika kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 21 Desemba, 2022 | 18 |
| Kielelezo Na. 4.1: | Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizindua Mwongozo wa Utoaji Elimu Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani, jijini Dar es Salaam tarehe 02 Julai, 2022 | 24 |
| Kielelezo Na. 5.1: | Idadi ya Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu kuanzia mwaka 2019 hadi Mwaka 2022 | 36 |

## MAELEZO YA WAZIRI

Tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuongezeka nchini na duniani kwa ujumla. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Jemedari wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kupambana na tatizo hilo kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015 pamoja na kufuata miongozo ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC).

Bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya inayolimwa na kutumiwa kwa wingi nchini katika mwaka 2022. Hekari 179 za mashamba ya bangi ziliteketezwa na tani 20.58 za dawa hiyo zilikamatwa katika mwaka 2022. Aidha, hivi karibuni, kumeibuka tabia ya kuchanganya bangi yenye kiasi kikubwa cha kilevi kwenye vyakula kama vile biskuti, asali, juisi, majani ya chai na keki. Tukiangalia Taarifa ya Dunia ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2022 utaona kuwa asilimia 40 ya nchi za wenzetu waliohalalisha matumizi ya bangi, zilikumbwa na idadi kubwa ya magonjwa ya afya ya akili yaliyosababishwa na matumizi ya dawa hiyo. Hali hii inalifanya Taifa letu liendelee kuharamisha bangi ili kuwakinga vijana wetu.

Operesheni za ukamataji wa dawa za kulevya nchini kwa mwaka 2022, zilifanikisha kukamata tani 15.2 za mirungi, kilo 254. 7 za heroin na kilo 1.7 ya cocaine. Aidha, kumekuwa na mwendelezo wa ukamataji wa dawa ya kulevya aina ya methamphertamine ambapo kwa mara ya kwanza zilikamatwa mwaka 2021 kiasi cha kilo 430.8 na kufuatiwa na mwaka 2022 ambapo gramu 968.7 zilikamatwa. Vilevile, mwaka 2022 umeshuhudia ukamataji wa dawa nyingine ngeni nchini inayojulikana kama mescaline ambapo gramu 56 zilikamatwa.

Kwa mara ya kwanza nchini, Serikali imefanikiwa kuandaa "*Mwongozo wa Utoaji Elimu Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini*" ili kuhakikisha jamii inapata elimu sahihi juu ya tatizo hili. Jitihada za kujengea uwezo walimu wa walimu zimeanza na tayari wahitimu kutoka asasi 27 za Mkoa wa Dar es Salaam wanaendelea kutoa elimu hiyo kwa makundi mengine. Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha elimu dhidi ya tatizo la dawa za kulevya inatolewa kwenye jamii.

Tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya iliendelea kutolewa ambapo kwa mwaka 2022 jumla ya waraibu 871,010 walinufaika na tiba hiyo nchini. Aidha, Serikali imeendelea kufadhili mafunzo ya stadi za kazi kwa waraibu wanaopata nafuu ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea.

Mafanikio haya ni matunda ya ushirikiano mkubwa baina ya wadau wa ndani na nje ya nchi pamoja na jamii kwa ujumla. Nawapongeza kwa jitihada hizi. Aidha, napenda kuwahimiza kila mtu kwa nafasi yake atimize wajibu katika kuhakikisha anatoa taarifa ya wanaojihusisha na kilimo au biashara ya dawa za kulevya na kuwasaidia wale waliopata uraibu kupata tiba.

Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb)

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**

## DIBAJI

Taarifa hii imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya Na 5 ya Mwaka 2015, ambacho kinailekeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya kuandaa na kuiwasilisha Bungeni. Lengo la taarifa ni kuitaarifu jamii juu ya hali ya tatizo la dawa za kulevya Nchini kwa mwaka 2022 pamoja na jitihada zilizofanyika katika kukabiliana nalo.

Taarifa hii imegawanyika katika sura saba. Sura ya kwanza inaonesha taswira ya tatizo la dawa za kulevya duniani kutoka kwenye Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2022. Sura ya pili inaelezea nguzo muhimu nne zinazotumika kupambana na tatizo la dawa za kulevya Nchini na mikakati yake. Nguzo hizo ni Kupunguza Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction), Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction), Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) na Kuimarisha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa (International Cooperation). Utekelezaji wa mikakati ya nguzo hizo umeainishwa katika sura ya tatu hadi ya sita.

Sura ya tatu imejikita kwenye kuelezea jitihada zilizofanyika katika Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya Nchini kwa mwaka 2022. Sura ya nne inaelezea utekelezaji wa nguzo ya Kupunguza Uhitaji (Matumizi) ya Dawa za Kulevya. Sura ya tano inaelezea utekelezaji wa nguzo ya Kupunguza Madhara yanayosababishwa na Matumizi ya Dawa za Kulevya Nchini. Sura ya sita inaelezea matukio ya ushirikishwaji miongoni mwa wadau wa mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Sura ya saba inatoa changamoto zilizojitokeza katika udhibiti wa dawa za kulevya nchini na mikakati yake.

Kwakuwa tatizo la dawa za kulevya ni mtambuka, linahitaji juhudi za pamoja katika kukabiliana nalo. Hivyo, natoa shukrani za pekee kwa wadau wote walioshiriki katika mapambano haya na kuwasilisha taarifa zao. Tuendeleze umoja wetu ili kuishinda vita hii na kufikia lengo la kuwa na Tanzania isiyojihusisha na dawa za kulevya.

Aretas J. Lyimo
**KAMISHNA JENERALI**
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA**
**KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# FAHARASA

| | |
|---|---|
| **ADEM** | Agency for the Development of Educational Management |
| **CBE** | College of Business Education |
| **CDC** | U.S Centers for Disease Control and Prevention |
| **CND** | Commission on Narcotic Drugs |
| **EU-ACT** | European Union Action against Drugs and Organized Crime |
| **GCLA** | Government Chemist Laboratory Authority |
| **GF** | Global Fund |
| **HONLEA** | Heads of National Drug Law Enforcement Agencies |
| **ICD** | Inland Container Depot |
| **INCB** | International Narcotics Control Board |
| **MAT** | Medication Assisted Treatment |
| **MSD** | Medical Stores Department |
| **NDC** | National Defence College |
| **PEPFAR** | The U.S President's Emergency Plan for AIDS Relief |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TAMISEMI** | Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TIC** | Tanzania Investment Centre |
| **TMDA** | Tanzania Medicines and Medical Devices Authority |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **UNODC** | United Nations Office on Drugs and Crime |
| **UVIKO** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |

# SURA YA KWANZA
# HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

## 1.1 Utangulizi

Katika kutoa taswira ya tatizo la dawa za kulevya duniani, Sura hii imetumia dondoo za Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022. Sura hii imeangazia matumizi, biashara, uzalishaji na matibabu kwa waraibu. Aidha, sura hii inaonesha jinsi janga la UVIKO linavyoendelea kuathiri matumizi, biashara, utoaji wa huduma kwa waraibu na udhibiti wa dawa za kulevya duniani.

## 1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani

Taarifa ya hali ya dawa za kulevya duniani ya mwaka 2022 ilionesha kuwa, matumizi ya dawa za kulevya yaliendelea kuongezeka duniani. Kulingana na taarifa hiyo inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 284 wenye miaka kati ya 15 hadi 64 walitumia dawa za kulevya duniani mwaka 2020. Idadi hii ni inafanya ongezeko la asilimia 26 toka mwaka 2010 ambapo ilikadiriwa kuwa watu waliotumia dawa za kulevya walikuwa milioni 226. Katika kipindi hicho, dawa za kulevya aina ya bangi, heroin, metamphetamine, cocaine pamoja na dawa tiba zenye asili ya kulevya zilitumika zaidi.

Katika kipindi hicho kulishuhudiwa ongezeko kubwa la uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa mpya za kulevya (New Psychotropic Substances-NPS) kuwahi kutokea duniani. Matumizi ya dawa za kulevya yaliripotiwa kusababisha madhara ya kiafya kwa watumiaji na jamii, kama vile ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI, magonjwa ya afya ya akili na homa ya ini. Hata hivyo jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kudhibiti uzalishaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya, ikiwa ni pamoja na utoaji wa tiba kwa waraibu wa dawa hizo.

### 1.2.1 Bangi

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, ilionesha kuwa bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumiwa zaidi duniani. Takribani watu milioni 209 walitumia bangi mwaka 2020, ikiwa ni sawa na asilimia nne (4) ya watu duniani kote, huku idadi ya watu wanaotumia bangi ikiongezeka kwa asilimia 23 katika muongo mmoja uliopita. Matumizi ya bangi yameendelea kuwa ya juu zaidi Amerika Kaskazini, ambapo asilimia 16.6 ya wakazi wanatumia dawa hiyo, huku ikiendelea kuwa dawa inayosumbua watu wengi wanaotibiwa barani Afrika. Pia taarifa hiyo ilionesha kuwa mwaka 2020, kilimo na ukamataji wa bangi duniani uliongezeka hadi kufikia rekodi ya juu zaidi.

Aidha, asilimia 40 ya nchi zilionesha kuwa idadi kubwa ya magonjwa ya afya ya akili yalisababishwa na matumizi ya bangi, na asilimia 33 zilionesha bangi kama dawa inayowasumbua zaidi hususani wale walio kwenye tiba za uraibu wa dawa za kulevya. Idadi kubwa zaidi ya watu wanaopatiwa tiba ya uraibu wa dawa za kulevya barani Afrika na baadhi ya nchi za Amerika ya Kusini na Caribbean, ni wale wanaotafuta usaidizi wa matatizo ya afya ya akili yanayosababishwa na matumizi ya bangi.

#### 1.2.1.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari Zake

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani 2022 ina viashiria vya awali vinavyoonesha kuwa uhalalishaji wa bangi katika maeneo ya Amerika Kaskazini na maeneo mengine umeleta athari kubwa hususani kwa afya ya jamii, usalama, mabadiliko ya masoko, ongezeko la biashara nyingine haramu (Usafirishaji haramu wa binadamu na biashara ya silaha za magendo) na kuathiri mapambano dhidi ya uhalifu. Bidhaa za bangi zimetofautiana ambapo viwango vya wastani vya kemikali inayosababisha uraibu kwenye bangi inayoitwa *Tetrahydrocannabinol* (THC) katika bidhaa mbalimbali za bangi kama biskuti na keki vimeendelea kuongezeka kufikia asilimia 60 kutoka kiwango cha asilimia tano (5) cha kemikali hiyo.

Taarifa kutoka Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (United Nations Office on Drugs and Crime-UNODC) ilionesha kuwa mitazamo hasi juu ya madhara ya bangi imeendelea kupungua katika maeneo yaliyohalalisha matumizi ya dawa hizo. Wakati huo huo, kumekua na ongezeko la watu walio na magonjwa ya afya ya akili na watu wanaojiua kutokana na matumizi ya bangi, ikiwa ni pamoja na idadi kubwa ya watu waliolazwa hospitalini kwa kuzidisha kiwango cha matumizi.

### 1.2.2 Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni

Dawa hizi zipo katika kundi la vipumbaza (depressant) na hutengezwa kutokana na mmea wa afyuni (opium poppy) kwa kuchakatwa na kemikali bashirifu, na hivyo kuzalisha dawa za kulevya aina ya heroin na morphine (opiates). Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, ilikadiriwa kuwa watu milioni 61 walitumia dawa za kulevya jamii ya afyuni mwaka 2020, ikiwa ni asilimia 1.2 ya idadi ya watu duniani. Takribani asilimia 40 ya waraibu waliokuwa kwenye tiba waliathiriwa zaidi na dawa za kulevya jamii ya afyuni, iliyosababisha theluthi mbili ya vifo vinavyohusiana moja kwa moja na kuzidisha matumizi ya dawa hiyo (overdoses).

Asilimia 86 ya uzalishaji haramu wa afyuni duniani umetokea nchini Afghanistan. Hata hivyo iliripotiwa kuwa njia ya Balkan ambayo huanzia nchi Afghanistan, Iran, Uturuki hadi Nchi za Ulaya imeendelea kuwa njia kuu ya usafirishaji wa dawa za kulevya jamii ya afyuni, huku ukamataji wa dawa zinazosafirishwa na watu binafsi ukiongezeka kwa mwaka 2021.

### 1.2.3 Cocaine

Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, ilikadiriwa kuwa watu milioni 21.5 walitumia cocaine mwaka 2020, ikiwa ni sawa na asilimia 0.4 ya idadi ya watu duniani. Katika taarifa hiyo ilionesha kuwa Amerika Kaskazini na Ulaya zimendelea kuwa masoko makuu ya biashara ya cocaine. Hata hivyo, iliripotiwa kuwa uhitaji wa dawa hiyo katika bara la Afrika na Asia umeongezeka maradufu katika miongo miwili iliyopita. Kiwango cha uzalishaji wa cocaine kilifikia rekodi ya juu zaidi mnamo mwaka 2020, ikifikia takribani tani 1,982, wakati ukamataji uliongezeka zaidi karibu na maeneo ya uzalishaji.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, inaonesha kuwa biashara na usafirishaji wa cocaine kwa njia ya bahari unazidi kushika kasi na karibu asilimia 90 ya kiasi cha cocaine kilichokamatwa kilihusishwa na shughuli za kiuchumi zinazofanyika baharini. Katika taarifa hiyo iliripotiwa kuwa soko la kimataifa la cocaine linazidi kupanuka na matumizi yamekuwa yakiongezeka duniani kote katika muongo uliopita. Kiasi kikubwa cha cocaine huzalishwa na husafirishwa kutoka Amerika Kusini hadi Ulaya kupitia Afrika Magharibi na Kaskazini. Hata hivyo, soko la cocaine limeongezeka zaidi nje ya maeneo yaliyozoeleka kwa biashara hiyo (Amerika Kaskazini, Ulaya Magharibi, Afrika na Asia).

### 1.2.4 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya ni dawa zinazotumika kutibu maradhi mbalimbali lakini, kutokana na asili yake ya kulevya, zikitumika bila kufuata ushauri wa daktari zinaweza kuleta uraibu. Taarifa ya Dunia ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2022, ilionesha kuwa ukamataji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya ulipungua kwa mwaka 2020, tofauti na hali ilivokuwa hapo awali. Hata hivyo, kupungua kwa ukamataji huo mwaka 2020, kulichangiwa zaidi na kushuka kwa utoaji wa taarifa.

Taarifa hiyo ilionesha kuwa ongezeko la matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya lilihusisha zaidi matumizi ya dawa aina ya Fentanyl huko Amerika Kaskazini na kusababisha ongezeko kubwa la vifo kuliko vilivyoshuhudiwa wakati wa janga la UVIKO. Barani Afrika kumekuwa na dalili za kuongezeka kwa matumizi yasiyo ya matibabu ya Tramadol katika nchi za Afrika Kaskazini na Afrika Magharibi. Vile vile matumizi hayo yalionekana kuongezeka pia katika nchi za Mashariki ya Kati na Kusini-Magharibi mwa Asia.

### 1.2.5 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances - NPS)

Dawa Mpya za Kulevya ni dawa zinazotengenezwa kwa kuiga kemikali zilizopo kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama vile bangi, heroin, mirungi na cocaine. Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, inaeleza kwamba hadi kufikia Desemba 2021, aina 1,127 za dawa mpya za kulevya zilitambuliwa na UNODC. Madhara ya NPS yanatofautiana kutoka dawa moja mpaka nyingine na yanaweza kujumuisha mabadiliko ya mtazamo, tabia na hisia.

Matumizi na usafirishaji haramu wa NPS ni suala la kimataifa, likiathiri zaidi nchi zilizoendelea. NPS mara nyingi huuzwa kwenye mitandao ya siri (Dark web), hivyo kuongeza urahisi wa upatikanaji wa dawa hizo. Taarifa ya UNODC ilionesha kuwa kati ya mwaka 2016 hadi 2020, ukamataji wa kiwango kikubwa cha dawa mpya za kulevya ulihusisha dawa aina ya vichangamshi (hususani Cathinone na Phenethylamines), zikifuatiwa na vileta njozi (Bangi, Tryptamines na baadhi ya Phenethylamines) na vipumbaza (hasa jamii ya Fentanyl).

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, ilionesha kuwa kuna ongezeko kubwa la matumizi ya NPS, hali ambayo imepelekea kuongezeka kwa changamoto za kiafya na kuongeza tishio la usalama kwa jamii. Taarifa hiyo imetoa wito kwa serikali


na mashirika ya udhibiti na usimamizi wa sheria ya dawa za kulevya duniani kuendelea kuchukua hatua za kukabiliana na matumizi pamoja na usafirishaji haramu wa NPS.

### 1.2.6 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetamine Type Stimulants-ATS)

Dawa za kulevya jamii ya Amphetamine ni kundi la dawa za kulevya linalojumuisha jamii mbalimbali za dawa ikiwemo amphetamine, methamphetamine na ecstasy. Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2022 imeonesha kuwa matumizi ya dawa za kulevya aina ya ATS yameendelea kuongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni. Katika taarifa hiyo ilionesha kuwa watumiaji wa amphetamine na methamphetamine waliongezeka zaidi duniani ikifikiwa takribani watu milioni 34 na watumiaji wa ecstasy pekee duniani wakifikia milioni 20.

Aidha, taarifa hiyo imeonesha kuwa zaidi ya tani 525 za ATS zilikamatwa mwaka 2020, hivyo kufanya ongezeko la asilimia 15 kwa kila mwaka kuanzia mwaka 2010 hadi 2020. Taarifa hiyo ilionesha kuwa ATS nyingi zaidi iliyokamatwa katika kipindi cha mwaka 2016-2020, ilihusisha dawa aina ya methampetamine, ikifuatiwa na amphetamine (asilimia 17) na ecstasy (asilimia 4), na asilimia zilizobaki zikihusisha ATS nyingine. Uzalishaji na biashara ya ATS imeendelea kuongezeka sambamba na maabara bubu ambazo zina uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa na kwa gharama ndogo.

Biashara ya ATS imetumiwa kufadhili shughuli nyingine za uhalifu kama vile biashara haramu ya silaha, ugaidi na biashara haramu ya binadamu. Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020, zaidi ya maabara bubu 16,000 zilizotumika kutengeneza ATS ziliharibiwa katika nchi 45 duniani, ambapo asilimia 69 ya maabara hizo zilijihusisha na utengenezaji wa methamphetamine.




**Kielelezo Namba 1.1 Watumiaji wa Dawa za Kulevya Duniani mwaka 2020**

## 1.3 Dawa za Kulevya na Jinsia

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022, ilionesha kuwa ingawa watu wengi wanaotumia dawa za kulevya ni wanaume, wanawake wameendelea kuonesha mahudhurio hafifu ya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya. Idadi kubwa ya watu wanaotumia dawa za kulevya imeendelea kuwa kubwa kwa wanaume, japokuwa asilimia 40 wanawake walitumia zaidi dawa za kulevya jamii ya Amphetamine (ATS) na dawa tiba zenye asili za kulevya. Taarifa hiyo ilionesha kuwa wanawake wanaotumia dawa za kulevya wanaathiriwa kwa haraka zaidi na magonjwa ya afya ya akili ikilinganishwa na wanaume.

Taarifa hiyo ilionesha kuwa kati ya watumiaji wawili wa dawa za kulevya jamii ya Amphetamine (ATS) mwaka 2021, mmoja alikuwa mwanamke, lakini ni mwanamke mmoja tu kati ya watano walipata tiba ya uraibu. Wanawake wanaotumia bangi wameongezeka ambapo asilimia tisa (9) ya wanawake walitumia bangi barani Asia na takribani asilimia 42 walitumia bangi Amerika Kaskazini. Barani Afrika kumekuwa na ongezeko kubwa la tofauti ya matumizi ya dawa za kulevya kati ya wanaume na wanawake, ambapo mwanamke mmoja kati ya wanaume tisa (09) alitumia bangi. Pia iliripotiwa kuwa idadi kubwa ya wanawake walitumia zaidi dawa za kulevya jamii ya afyuni ikilinganishwa na dawa nyingine.

## 1.4 Dawa za Kulevya na UVIKO 19

Kulingana na Taarifa ya Dunia ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2022, ilibaini kuwa janga la UVIKO-19 liliendelea kuleta mabadiliko katika mbinu za biashara na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Katika kipindi cha kufungiwa (lockdown) kilichosababishwa na janga la UVIKO-19, kilichochea ongezeko la matumizi ya bangi kwa mwaka 2020.

Katika mwaka 2020, kulikuwa na upatikanaji mdogo wa huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa nchi zote duniani. Kuibuka kwa janga la UVIKO-19, kuliwaathiri zaidi watu waliokuwa wanapata tiba ya uraibu kwa kukosa huduma hizo na kusababisha ongezeko la madhara ya dawa za kulevya. Katika kipindi hicho kumeshuhudiwa ongezeko kubwa kuwahi kutokea la kurudia matumizi ya dawa za kulevya (relapse) kwa watu waliokuwa wakipata tiba ya uraibu katika vituo mbalimbali. Ongezeko hilo liliambatana na kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazohusiana na matumizi ya dawa za kulevya.

# SURA YA PILI

## MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

### 2.1 Utangulizi

Tanzania imeendelea kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015 pamoja na kufuata miongozo ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC). Serikali imeendelea kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kuzingatia nguzo kuu nne ambayo ni; ni kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya (supply reduction), kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya (demand reduction), kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya (harm reduction) na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa (international cooperation). Sura hii inatoa taswira ya nguzo hizo ili kutoa mwongozo kwa sura zinazofuata.

### 2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)

Lengo la nguzo hii ni kudhibiti uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini. Upatikanaji wa dawa za kulevya unahusisha kilimo, utengenezaji, uingizaji na usambazaji kupitia mipaka ya nchi kavu, majini na anga. Katika utekelezaji wa nguzo hii, mikakati ifuatayo huzingatiwa; Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa kuhusu biashara ya dawa za kulevya, ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya, usimamiaji wa sheria ya dawa za kulevya nchini, udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kuratibu uteketezaji wa dawa za kulevya.

### 2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)

Nguzo hii inazingatia utoaji wa elimu kama mkakati muhimu wa kuifanya jamii kujitambua na kujiepusha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini.

Katika utekelezaji wa nguzo hii Mamlaka inaratibu uelimishaji juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii, ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo ya uelimishaji, kuwaandaa na kuwawezesha watoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya, kuratibu asasi zinazotoa elimu ya dawa za kulevya kwa umma, kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa klabu za dawa za kulevya na kuhuisha maudhui ya dawa za kulevya kwenye mitaala ya elimu.

### 2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction)

Katika utekelezaji wa nguzo hii, utoaji wa huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya ni moja ya mkakati muhimu wa kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo. Mraibu ni mgonjwa kama wagonjwa wengine, hivyo uraibu wa dawa za kulevya ni tatizo la kiafya na huathiri watumiaji na jamii. Tiba ya uraibu na magonjwa yanayoambatana ni muhimu ili kuwakinga watumiaji wa dawa za kulevya na jamii. Aidha, mikakati mingine ni kuratibu matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya, kuandaa miongozo ya matibabu, kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba na unasihi na kutoa elimu ya kupunguza madhara.

## 2.5 Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Lengo la nguzo hii ni kuunganisha nguvu ya pamoja katika mapambano na udhibiti wa dawa za kulevya kitaifa, kikanda na kimataifa. Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka linalohusisha mitandao ya kihalifu iliyopo nchi mbalimbali duniani, hivyo mapambano dhidi ya tatizo hili yanahitaji ushirikiano na nguvu za pamoja kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Katika utekelezaji wa nguzo hii, mikakati ifuatayo inazingatiwa; kubadilishana taarifa za kiintelejensia na uzoefu baina ya mataifa kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya, kutekeleza mikataba na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya, kuhudhuria mikutano na mafunzo kuhusu udhibiti wa dawa hizo, pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika mapambano hayo.

# SURA YA TATU
# KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea jitihada zilizofanyika katika kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya nchini kwa mwaka 2022. Jitihada hizi zilifanyika kwa ushirikiano mkubwa baina ya vyombo vya udhibiti ikiwemo Interpol, Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa na wananchi.

## 3.2 Udhibiti wa Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Mamlaka ikishirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi imefanikiwa kukamata dawa za kulevya za mashambani kama vile bangi na mirungi pamoja na dawa zilizozalishwa viwandani ambazo ni heroin, cocaine na methamphetamine. Mafanikio ya udhibiti wa dawa hizo yameainishwa kama ifuatavyo: **-**

**Bangi**

Kiasi cha tani **20.58** za bangi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa **10,277**, wanaume **9,549** na wanawake **728.** (***Kielelezo Na. 3.1 na Kielelezo Na.3.2).***


Katika miaka ya hivi karibuni, bangi imeanza kutumika katika utengenezaji wa vyakula mbalimbali kama vile biskuti, asali, juisi, majani ya chai na keki. Aidha, mwaka 2022 watuhumiwa watatu walikamatwa wakihusishwa na usambazaji wa bidhaa hizo.

**Mirungi**

Kiasi cha tani **15.23** za mirungi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa **1,491** kati yao wanaume **1,327** na wanawake **164**. **(*Rejea Kielelezo Na.3.1 na Kielelezo Na.3.2).***

**Jedwali Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kwa muongo mmoja (mwaka 2013 -2022)**

| Mwaka | Bangi (Tani) | Mirungi (Tani) |
|---|---|---|
| **2013** | 85.80 | 12.82 |
| **2014** | 81.30 | 15.74 |
| **2015** | 22.01 | 16.60 |
| **2016** | 68.23 | 21.64 |
| **2017** | 52.19 | 67.81 |
| **2018** | 24.30 | 8.96 |
| **2019** | 21.51 | 9.07 |
| **2020** | 13.23 | 11.80 |
| **2021** | 22.74 | 10.93 |
| **2022** | 20.58 | 15.23 |





**Kielelezo Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2013-2022**

Takwimu katika jedwali namba 3.1 na chati namba 3.1 zinaonesha kuwa kiasi cha bangi na mirungi kilichokamatwa kiliendelea kupungua kuanzia mwaka 2018 mpaka 2022 hii ni kutokana na kuimarika kwa jitihada za udhibiti na ukamataji. Hata hivyo juhudi zaidi zinaendelea katika kutoa elimu na ukamataji ili kufikia maeneo mengi ya uzalishaji.

**Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2013-2022**

| Mwaka | Watuhumiwa – Bangi | Watuhumiwa – Mirungi |
|---|---|---|
| **2013** | 1,547 | 581 |
| **2014** | 11,918 | 1,650 |
| **2015** | 13,275 | 1,780 |
| **2016** | 17,889 | 2,397 |
| **2017** | 11,528 | 1,797 |
| **2018** | 9,744 | 1,185 |
| **2019** | 8,865 | 1,170 |
| **2020** | 7,601 | 1,156 |
| **2021** | 9,484 | 1,395 |
| **2022** | 10,277 | 1,491 |




**Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa kwa Kujihusisha na Bangi na Mirungi Nchini Kati ya Mwaka 2011 – 2020**

Kielelezo Na. 3.3 na 3.4 kinaonesha idadi ya watuhumiwa wa bangi na mirungi kwa mwaka 2022 imeendelea kupungua ikilinganishwa na miaka iliyopita hii ni kutokana na juhudi kubwa zinazofanyika katika udhibiti. Hata hivyo kupungua kwa watuhumiwa kumechangiwa adhabu kali zinazotolewa pamoja na elimu inayoendelea kutolewa kuhusu dawa za kulevya.

**Heroin**

Jumla ya kilo 254.71 za heroin zilikamatwa nchini mwaka 2022 zikiwahusisha watuhumiwa 409, wanaume 391 na wanawake 18. (*Rejea kielelezo 3.5 Na. 3.6 na Kielelezo Na. 3.7)*.


**Cocaine**

Kiasi cha kilo 1.73 za cocaine zilikamatwa zikiwahusisha watuhumiwa 122, wanaume 118 na wanawake wanne (4). (*Rejea kielelezo 3.5 Na. 3.6)*.

**Jedwali Na. 3.3: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Katika muongo mmoja (Mwaka 2013-2022)**

| Mwaka | Kiasi cha Heroin kilichokamatwa (Kg) | Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa (Kg) |
|---|---|---|
| **2013** | 36 | 4 |
| **2014** | 400 | 45 |
| **2015** | 64.75 | 17.79 |
| **2016** | 42.26 | 18.52 |

| | | |
|---|---|---|
| **2017** | 185.56 | 4.14 |
| **2018** | 16.94 | 7.67 |
| **2019** | 55.35 | 10.34 |
| **2020** | 349.81 | 4.52 |
| **2021** | 1,124.52 | 0.81 |
| **2022** | 254.71 | 1.73 |




**Kielelezo Na. 3.3: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2013-2022**


Takwimu zinaonesha kuwa kiasi cha heroin kilichokamatwa kwa mwaka 2022 kilishuka zaidi ikilinganishwa na mwaka 2021. Hali hii inatokana na juhudi za ukamataji uliohusisha wafanyabiashara wakubwa wa dawa hizo kwa mwaka 2021. Aidha, Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha cocaine kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2021, kutokana na mbinu mpya za usafirishaji. Hata hivyo juhudi zinaendelea kufanyika kuhakikisha kuwa kiasi hicho kinazidi kupungua zaidi hapa nchini.



**Kielelezo Na. 3.4: Shehena ya kilo 859.36 za dawa za kulevya zikijumuisha kilo 504.36 za heroin na kilo 355 za methamphetamine zilizokamatwa Bahari ya Hindi eneo la Kilwa Masoko, mkoani Lindi**

**Jedwali Na. 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa katika muongo mmoja (Mwaka 2013-2022)**

| Mwaka | Heroin | Cocaine |
|---|---|---|
| **2013** | 75 | 20 |
| **2014** | 584 | 351 |
| **2015** | 474 | 281 |
| **2016** | 716 | 263 |
| **2017** | 1,005 | 243 |
| **2018** | 463 | 148 |
| **2019** | 318 | 31 |
| **2020** | 428 | 80 |
| **2021** | 588 | 100 |
| **2022** | 409 | 122 |




**Kielelezo Na. 3.5: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa kati ya Mwaka 2013 - 2022**

Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na Heroin na Cocaine kwa mwaka 2022 iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2021. Ongezeko hili

linatokana na ushirikiano uliopo kati ya jamii na vyombo vya dola katika upatikanaji wa taarifa uliosaidia ukamatwaji kwa watuhumiwa hao.

**Dawa Nyingine za Kulevya**

Katika kipindi cha mwaka 2021, dawa za kulevya aina ya methamphetamine kiasi cha kilo 430.77 kilikamatwa kwa mara ya kwanza zikihusisha watuhumiwa tisa (9). Dawa hii imeendelea kukamatwa hapa nchini hali inayodhihirisha kuwepo kwa biashara ya dawa hii. Kwa mwaka 2022 kiasi cha gramu 968.7 kilikamatwa kikihusisha watuhumiwa wawili (2). Juhudi zinaendelea kuhakikisha kuwa biashara ya dawa hii inatokomezwa kabisa nchini. Aidha, kwa mara ya kwanza dawa za kulevya aina ya mescaline gramu 56.04 zilikamatwa zilizohusisha mtuhumiwa moja (1). Hatahivyo, matumizi ya dawa hizi bado hayajathibitishwa hapa nchini.

**Jedwali Na. 3.5: Kiasi cha methamphetamine na mescaline kilichokamatwa mwaka 2021 - 2022**

| Na. | Mwaka | Methamphetamine (Kilo) | Mescaline (Gramu) |
|---|---|---|---|
| 1 | 2021 | 430.77 | - |
| 2 | 2022 | 0.97 | 56 |

## 3.4 Watuhumiwa wa dawa za kulevya waliokamatwa nje ya nchi

Baadhi ya watanzania wameendelea kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya katika nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi cha mwaka 2022, watanzania 147 walikamatwa nje ya nchi wakituhumiwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya, kati yao wanawake walikuwa 11 na wanaume walikuwa 136.

## 3.5 Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)

Kemikali bashirifu zina matumizi halali muhimu kama zilivyo kemikali nyingine ambazo hutumika katika shughuli za uzalishaji viwandani kama malighafi. Kemikali hizi pia ni malighafi za kutengeneza dawa za kulevya, hivyo wahalifu huweza kuzichepusha na kuziingiza katika utengenezaji wa dawa hizo. Kemikali bashirifu zinahitaji ufuatiliaji na ukaguzi unaoambatana na utoaji elimu ili kudhibiti uwezekano wa kuchepushwa na kutumika kutengeneza dawaza kulevya.

Kemikali hizi huingia nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya Mwaka 2003. Udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali hizo hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015. Jukumu hilo hutekelezwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa ushirikiano wa karibu na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Katika kipindi cha mwaka 2022, kiasi cha tani 11,389 na lita za ujazo 5,711,266 za kemikali hizo ziliingizwa nchini kwa kufuata utaratibu wa kisheria. Aidha, kiasi cha tani 102.7 na lita za ujazo 972,210 zilisafirishwa nje ya nchi. Kemikali zilizosambazwa kwa matumizi ya ndani ya nchi ni tani 6,780 na lita 6,403,568. Jedwali namba 3.6

linainisha kemikali bashirifu zilizoingizwa nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2022.

**Jedwali Na. 3.6: Mwenendo wa Uingizaji wa Kemikali Bashirifu Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2022**

| Mwaka | Idadi ya Kampuni | Kiasi cha Kemikali | |
|---|---|---|---|
| | | Tani | Lita |
| 2017 | 167 | 116,257.00 | 13,016,466.00 |
| 2018 | 184 | 1,534,064.00 | 11,247,555.00 |
| 2019 | 160 | 249,768.00 | 6,304,971.00 |
| 2020 | 87 | 96,062.44 | 4,256,161.00 |
| 2021 | 57 | 3,655.97 | 855,807.00 |
| 2022 | 94 | 11,389.00 | 5,711,266.00 |

*Chanzo: Taarifa za mwaka za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali*

Takwimu zinaonesha kwamba, katika kipindi cha mwaka 2022, uingizwaji wa kemikali bashirifu uliongezeka kwa wastani wa asilimia 76 ikilinganishwa na mwaka 2021, hali inayotokana na kuongezeka kwa mahitaji yake.

### 3.6 Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Kemikali Bashirifu

Ukaguzi na ufuatiliaji hufanyika ili kudhibiti mianya ya uchepushaji wa kemikali hizo katika maeneo mbalimbali ikiwemo bandari, vituo vya forodha vya mipakani, kampuni zinazofanya biashara ya kemikali na kampuni au taasisi zinazohusika na usafirishaji wa vifurushi ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2022, ukaguzi na ufuatiliaji ulifanyika kwa kampuni 56 za kemikali katika mikoa ya Tanga, Geita, Mbeya, Dar es Salaam, Pwani, Shinyanga, Manyara, Mtwara, Arusha na Mwanza. Pia, vituo saba (7) vya forodha katika mipaka ya Namanga, Kilambo, Horohoro, Mtambaswala, Mkenda, Kasumulo na Tunduma vilikaguliwa. Vile vile, ukaguzi na ufuatiliaji ulifanyika katika bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Kasanga na bandari kavu (ICDs) tano za GALCO, AZAM, AFICD, PMM na AFS pamoja na kampuni za usafirishaji wa vifurushi kama vile DHL, SWISS PORT, ARAMEX, FEDEX, POSTA, UPS na Nitume.

Kupitia kaguzi na ufuatiliaji uliofanyika, ilibainika kuwepo kwa usafirishaji haramu wa lita 25,000 za kemikali bashirifu na baadhi ya kampuni kufanya biashara bila usajili kwa mujibu wa sheria. Kaguzi hizo zilibaini udanganyifu wa nyaraka zinazoambatishwa katika mfumo unaoratibu uingiaji na utoaji wa mizigo nchini.

Aidha, kiasi cha tani 98.29 na lita 85 za kemikali bashirifu zilizuliwa kuingizwa nchini kwa kutumia mifumo ya kimataifa ya udhibiti wa kielektroniki, kwa kuwa hazikukidhi matakwa ya sheria za nchi na kimataifa. Kemikali hizo ni phenyl acetic acid, toluene, acetone, methyl ethyl ketone, sulphuric acid na pseudoephedrine hydrochloride.

**Jedwali Na. 3.7: Kiasi cha Kemikali Bashirifu kilichozuiliwa kuingia nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2022**

| Mwaka | Tani | Lita |
|---|---|---|
| **2017** | 250.1 | - |
| **2018** | 23.1 | - |
| **2019** | 43.6 | - |
| **2020** | 57.6 | - |
| **2021** | 120.3 | - |
| **2022** | 98.3 | 85 |

### 3.7 Udhibiti wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya hutumika katika tiba mbalimbali kwa wahitaji na hutolewa kwa maelekezo maalum ya daktari. Kwa kuwa dawa hizi zina uwezo wa kulevya na kusababisha uraibu, huweza kuchepushwa na kutumika, hivyo kuathiri afya ya mtumiaji na jamii yake. Dawa hizo ni pamoja na Pethidine, Fentanyl, Morphine, Tramadol, Ketamine, Benzodiazepines (Diazepam, Xanax, Lorazepam), Codeine na Phenobarbitone.

Katika kuepusha jamii na madhara ya dawa hizi Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA) husimamia uagizaji na matumizi ya dawa hizi zilizopo kwenye orodha ya dawa zinazodhibitiwa ili zitumike kwa mujibu wa taratibu za kitabibu chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba (Sura 219). Mamlaka kwa kushirikiana TMDA imeendelea kudhibiti uchepushaji wa dawa hizi kwa kuzingatia Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015.

### 3.8 Uchunguzi wa Kimaabara wa Dawa za Kulevya

Uchunguzi wa kimaabara wa dawa za kulevya ni takwa la kisheria ili kuthibitisha aina za dawa za kulevya zinazokamatwa. Katika kipindi cha Mwaka 2022, jumla ya sampuli 166,451 zilifikishwa na kufanyiwa uchunguzi, katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kati ya hizo, asilimia 99.56 zilibainika kuwa ni dawa za kulevya ambapo dawa aina ya bangi iliongoza kwa wingi wa sampuli kwa asilimia 84.1 ikifuatiwa na mirungi asilimia 12.9. Mchanganuo wa sampuli za dawa za kulevya zilizochunguzwa katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umeainishwa katika Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Na. 3.8: Sampuli za Dawa za Kulevya zilizofanyiwa Uchunguzi Mwaka 2022**

| Dawa za kulevya | Idadi ya Sampuli | Asilimia |
|---|---|---|
| **Bangi** | 140,055 | 84.141% |
| **Mirungi** | 21516 | 12.926% |
| **Heroin** | 4251 | 2.554% |
| **Psychotropics (Diazepam, Lorazepam, Clonazepam)** | 38 | 0.023% |
| **Cocaine** | 15 | 0.009% |
| **Methamphetamine** | 10 | 0.006% |
| **Mchanganyiko** | 493 | 0.296% |
| **Ambazo siyo dawa za kulevya** | 73 | 0.044% |
| **Jumla** | **166451** | **99.999%** |

### 3.9 Kaguzi zilizofanyika katika Kudhibiti Dawa Tiba zenye asili ya Kulevya

Kwa mwaka 2022 ukaguzi ulifanyika kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za udhibiti nchini katika maeneo 84 yakihusisha maduka ya dawa za binadamu kwenye mikoa ya Geita, Mwanza, Mbeya, Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga na Manyara. Aidha, ukaguzi ulifanyika katika vituo saba (7) vya forodha katika mipaka ya Namanga, Kilambo, Horohoro, Mtambaswala, Mkenda, Kasumulo na Tunduma. Vilevile, ukaguzi ulifanyika katika kampuni za usafirishaji vifurushi zinazopitisha mizigo yake katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere pamoja na Shirika la Posta Dar es Salaam.

Ukaguzi huo ulibaini uingizwaji haramu ya dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Morphine (chupa 250), Pethidine (chupa 670) na Fentanyl (chupa 4,260) zikitokea katika nchi jirani. Vile vile, ilibainika kutokuwepo kwa baadhi ya kumbukumbu za manunuzi na mauzo ya dawa iliyoashiria uwepo wa mianya ya uchepushwaji wa dawa hizo na hatua za kisheria zilichukuliwa kwa wahusika. Aidha, kaguzi zilienda sambamba na uchunguzi wa matumizi haramu ya dawa tiba zenye asili ya kulevya zilizofanyika katika mikoa ya Mbeya, Geita na Mwanza. Matokeo ya uchunguzi yalidhihirisha uwepo wa matumizi ya dawa tiba zenye udhibiti maalum za Tramadol, Diazepam (Valium) na Phenobarbitone kwenye mikoa hiyo.

### 3.10 Maboresho ya Sheria

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015 imekuwa ikifanyiwa marekebisho kulingana na changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Miongoni mwa maboresho yaliyofanyika mwaka 2022 ni kufutwa na kuandikwa upya kwa kifungu cha 32 cha sheria ambapo katika maboresho hayo kwa sasa Afisa wa Mamlaka anakuwa na uwezo wa kufanya upekuzi muda wowote katika masaa 24 ya siku. Kifungu hicho pia kimempa Kamishna Jenerali mamlaka ya kutoa Hati ya Upekuzi (Search order) ambayo hapo awali ilikuwa inatolewa na Mkuu wa Kituo cha Polisi pekee chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20.

Maboresho mengine yaliyofanyika ni kuipa Mamlaka uwezo wa kuanzisha mahabusu na kuhifadhi watuhumiwa wa kesi za dawa za kulevya katika kipindi cha upelelezi. Mabadiliko haya yamelenga katika kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kujenga jamii ya kitanzania isiyojihusisha na dawa za kulevya.

### 3.11 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya

Mwaka 2022 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilifanya uteketezaji wa Dawa za Kulevya kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilifanyika mwezi Februari 2022 ambayo ilihusisha uteketezwaji wa kilo 250.7 za dawa za kulevya zilizojumuisha kilo 51.7 za Heroin na kilo 199 zenye mchanganyiko wa heroin na cocaine katika kiwanda cha Saruji cha Dangote mkoani Mtwara.

Awamu ya pili ilifanyika mwezi Disemba 2022 ambapo jumla ya tani 2.6 za dawa za kulevya zilizojumuisha tani mbili (2) za bangi na mirungi, kilo 569.3 za heroin na kilo 15.3 za cocaine ziliteketezwa katika kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill jijini Dar es Salaam. Aidha, jumla ya hekari 179 za mashamba ya bangi ziliteketezwa nchini katika kipindi hicho. Uteketezaji huu una lengo la kuhakikisha kuwa dawa hizo haziingii katika matumizi na biashara haramu. Dawa za Kulevya zinazokamatwa huteketezwa kwa mujibu wa sheria kwa kushirikisha Mamlaka mbalimbali za Serikali baada ya maamuzi kutolewa na Mahakama.



**Kielelezo Na. 3.6: Zoezi la uteketezaji wa dawa za kulevya lililofanyika katika kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 21 Desemba, 2022**

### 3.12 Kesi za Dawa za Kulevya

Mwaka 2022 umekuwa wa mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya ambapo jumla ya kesi 9,865 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Kesi hizo zipo katika mchanguo kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 3.14

**Jedwali Na. 3.9: jumla ya kesi zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini**

| Kundi la dawa | Aina ya dawa | Kesi zilizoripotiwa |
|---|---|---|
| **Dawa za viwandani** | Heroin | 347 |
| | Cocaine | 111 |
| | Methamphetamine | 2 |
| | Mescaline | 1 |
| | **Jumla** | **461** |
| **Dawa za mashambani** | Bangi | 8,031 |
| | Mirungi | 1,373 |
| | **Jumla** | **9,404** |

# SURA YA NNE
# KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea utekelezaji wa nguzo ya kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau imejikita kwenye utoaji elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ili jamii isijiingize katika matumizi ya dawa hizo. Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya hutolewa kwa jamii kupitia vyombo vya habari, machapisho, semina, makongamano na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa.

## 4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya ni kemikali ambazo huathiri mfumo wa fahamu na kubadilisha fikra, hisia na tabia za mtumiaji na hupelekea kutenda matendo ambayo hayakubaliki na jamii inayomzunguka. Dawa za kulevya zinazoongoza kwa matumizi nchini Tanzania ni bangi ikifuatiwa na heroin, mirungi na cocaine. Lakini katika miaka ya hivi karibuni kumeibuka matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kutokana na kuadimika kwa dawa za kulevya walizokuwa wanazitumia pamoja na matumizi ya viyeyushi aina ya gundi na petroli. Aidha, kumekuwepo na uingizwaji wa dawa za kulevya aina ya methamphetamine, lakini bado matumizi yake hayajathibitishwa nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2022, dawa za kulevya zimeendelea kuwa tatizo kubwa miongoni mwa wanajamii hali inayopelekea kuongezeka kwa matukio mengi ya kihalifu na mmomonyoko wa maadili katika jamii.

### 4.2.1 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya

Kwa miaka mingi serikali imekuwa ikifanya jitihada nyingi katika kuiepusha jamii kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Hatahivyo, tatizo la matumizi ya dwa za kulevya limeendelea kuisumbua jamii hasa vijana. Sababu zinazosababisha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa jamii ni kama ifuatavyo: -

**a. Urahisi wa upatikanaji wa dawa za kulevya**

Baadhi ya dawa za kulevya kama vile bangi na mirungi zimekuwa zikipatikana kwa urahisi katika mazingira yetu. Hali hii imekuwa ni miongoni mwa sababu ya watu wengi kushawishiwa na kujiingiza katika matumizi ya dawa hizo.

**b. Msukumo rika na kufuata mkumbo**

Baadhi ya vijana hujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kutokana na ushawishi wa vijana wenzao wa rika moja wanaotumia dawa hizo. Aidha, kuishi na mwenza, mpenzi au ndugu ambaye anajihusisha na matumizi ya dawa za kulevya huchangia katika kuanza matumizi ya dawa hizo.

**c. Ukuaji wa teknolojia**

Matumizi ya utandawazi na mitandao ya kijamii vimechangia jamii kuiga tamaduni potofu za kigeni, ikiwemo kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

**d. Migogoro ya kifamilia**

Utengano wa kifamilia unaweza kusababisha kukosekana kwa malezi bora na uangalizi wa karibu hivyo kupelekea watoto na vijana wengi kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya.

**e. Kukosa stadi za maisha**

Hali ya jamii kukosa uwezo wa kutambua changamoto zao na njia sahihi ya kuzitatua. Mfano, vijana kutokujishughulisha kujiingizia kipato imesababisha kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya.

**f. Imani potofu**

Baadhi ya mila na desturi katika jamii zimekuwa zikichangia matumizi ya dawa za kulevya nchini. Mfano, watu huamini wakitumia bangi hupata nguvu za kufanya kazi zaidi ikiwepo kulima, kusoma au kuimba na kucheza bila kuona aibu.

**g. Uelewa mdogo juu ya madhara ya dawa za kulevya**

Kundi kubwa la watu hujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kujifurahisha, kustarehe na kupunguza ukali wa maisha bila kufahamu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya.

**h. Matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya bila kufuata ushauri wa daktari**

Dawa tiba zenye asili ya kulevya zinapotumiwa mara kwa mara na bila kufuata ushauri wa daktari husababisha uraibu. Mfano, dawa za kutuliza maumivu ya mwili na usingizi (Valium, Tramadol au Morphine)

**i. Magonjwa ya akili**

Magonjwa kama saikosisi (kuchanganyikiwa), msongo wa mawazo, sonona na kihoro yanachangia baadhi ya watu kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Hii hutokana na watu wenye magonjwa ya afya ya akili kutumia dawa za kulevya kama njia ya kustahimili magonjwa hayo.

**j. Kurithi vinasaba vya uraibu**

Kuwepo kwa vinasaba vya uraibu kwa mmoja wa mzazi wa mtoto huchangia mtoto anayezaliwa kuwa na hali ya uraibu. Hata hivyo, tafiti zinaendelea kuthibitisha hili.

## 4.3 Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha madhara mbalimbali katika jamii kama vile; kiafya, kijamii, kiuchumi, kimazingira na unyanyapaa. Madhara hayo yameainishwa kama ifuatavyo; -

### 4.3.1 Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya humweka mtumiaji katika hatari ya kupata magonjwa ya akili, uraibu, moyo, shinikizo la damu na kiharusi. Dawa hizo zinapotumika kwa njia ya kujidunga huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini hasa aina B na C na kifua kikuu miongoni mwa watumiaji. Mtumiaji hupata arosto anapokosa kutumia dawa za kulevya na kujikuta anakuwa mraibu wa dawa hizo.

Aidha, matumizi ya dawa za kulevya hupunguza kumbukumbu, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi. Pia, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga pale wanapotumia kiasi kikubwa cha dawa za kulevya (overdose).

Madhara mengine ya kiafya ni pamoja na saratani, upungufu wa nguvu za kiume, kukosa usingizi, kukosa hamu ya kula na kuoza meno. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ulemavu na upungufu wa kinga ya mwili dhidi ya maradhi. Dawa za kulevya kwa wanawake huvuruga mtiriko wa hedhi, huharibu mimba, husababisha kuzaliwa kwa watoto wenye uraibu wa dawa za kulevya, waliodumaa kimwili na kiakili, matatizo ya moyo, ulemavu wa viungo au kujifungua watoto njiti. Kwa ujumla matumizi ya dawa hizi hupunguza umri wa kuishi wa mtumiaji kutokana na maradhi, uhalifu au kuzidisha kiasi cha dawa (overdose).

### 4.3.2 Kijamii

Waraibu wa dawa za kulevya kwenye jamii husababisha kukithiri kwa vitendo vya kihalifu ikiwemo wizi, ukahaba, utapeli na uporaji kwa ajili ya kupata fedha za kununulia dawa hizo. Matumizi ya dawa za kulevya huvuruga mahusiano katika familia na kusababisha kutengana kwa wazazi, kutelekeza familia hivyo watoto kukosa malezi bora na kukimbilia mitaani. Pia, matumizi ya dawa za kulevya kwa wanafunzi huathiri maendeleo ya mwanafunzi shuleni na kusababisha utoro, utovu wa nidhamu na hata kufukuzwa shule.

Dawa za kulevya huchangia ongezeko la maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu katika jamii kutoka kwa watumiaji ambao huwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya maradhi hayo. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazoweza kuepukika ambazo husababisha ulemavu, vifo, uharibifu wa mali na miundombinu.

### 4.3.3 Kiuchumi

Matumizi ya dawa za kulevya hupunguza ufanisi kazini na kusababisha kupoteza ajira au kufilisika. Mtumiaji hushindwa kuajirika hivyo kusababisha umaskini kwake, jamii yake na Taifa kwa ujumla. Aidha, waraibu wa dawa za kulevya ambao wengi ni vijana hujikuta wakishindwa kujihusisha na shughuli za uzalishaji mali na hupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Serikali huingia gharama zisizo za lazima kwa ajili ya tiba ya waraibu na kutoa elimu. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya yanaambatana na uhalifu unaoweza kusababisha kufungwa gerezani hivyo, serikali kuingia gharama za kuwahudumia wafungwa hao badala ya kuelekeza rasilimali hizo kwenye shughuli za maendeleo.

### 4.3.4 Kimazingira

Wajidunga wa dawa za kulevya husababisha uchafuzi wa mazingira pale sindano zilizotumika zinapotupwa kwenye vichochoro, viwanja vya michezo, fukwe na vituo vya daladala. Wavutaji wa dawa za kulevya huchafua hewa kwa moshi unaotoka kwenye dawa hizo na kudhuru afya za watu walio karibu nao.

#### 4.3.5 Unyanyapaa

Waraibu wa dawa za kulevya wamekua wakinyanyapaliwa na familia zao pamoja na jamii kwa ujumla, hivyo husababisha wakose haki zao hata pale wanapoacha matumizi ya dawa hizo. Mfano, kukosa urithi, ajira na kusingiziwa makosa. Unyanyapaa huo huwafanya waraibu wengi kutojithamini na kuwa na hofu ya kushiriki kwenye shughuli na huduma za jamii ikiwemo kushindwa kuhudhuria kwenye vituo vya afya kupata matibabu. Aidha, kutokana na unyanyapaa huo waraibu walioacha kutumia dawa za kulevya wanarudi kwenye makundi ya wenzao kutafuta faraja, hivyo wanajikuta wanarejea katika matumizi ya dawa hizo.

### 4.4 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya

Katika kipindi cha mwaka 2022 jitihada mbalimbali za kutoa elimu zilifanywa na Mamlaka na wadau katika kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya.

#### 4.4.1 Kazi za Uelimishaji zilizofanywa na Mamlaka

**i. Uzinduzi na Mafunzo ya Mwongozo wa Utoaji Elimu**

Katika kuhakikisha elimu juu ya dawa za kulevya inatolewa kwa viwango na inawafikia Watanzania wengi zaidi, Mamlaka iliandaa "*Mwongozo wa Utoaji Elimu Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini".* Awamu ya kwanza ya mafunzo kwa "*Walimu wa Mwongozo"* yalitolewa kwa Asasi za kiraia 27 za jiji la Dar es Salaam. Wahitimu waliopekea mafunzo kutoka kwenye asasi hizo wanatarajiwa kutoa elimu hiyo katika maeneo yao ya kiutendaji na kuifikia jamii kubwa zaidi.



**Kielelezo Na. 4.1: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizindua Mwongozo wa Utoaji Elimu Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani, jijini Dar es Salaam tarehe 02 Julai, 2022**

**ii Taasisi za Serikali**

Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa watumishi na wanavyuo wapatao 3,000 kutoka katika vyuo vifuatavyo; Chuo cha Elimu ya Biashara kampasi ya Dar es Salaam (CBE); Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Dar es Salaam; Chuo cha Wakala wa Maendeleo ya Elimu (ADEM) Pwani na Chuo cha Mipango Dodoma. Aidha, Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa watumishi katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili kutumia ujuzi huo kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

**iii Vyombo vya Habari**

Mamlaka ilitumia vyombo vya habari kufikisha elimu ya tatizo la dawa za kulevya kwa Umma. Elimu hiyo ilitolewa kupitia vituo vya redio, runinga, magazeti, vipeperushi, majarida, mitandao ya kijamii na tovuti ya Mamlaka. Mamlaka imefanikiwa kutoa elimu kwa waandishi wa habari katika redio 12 za kijamii katika Kanda ya Kusini inayojumuisha mikoa ya Lindi na Mtwara. Wasikilizaji wa kanda hiyo iliyokithiri kwa usafirishaji mkubwa wa dawa za kulevya walipata uelewa wa madhara ya dawa hizo na kuhamasishwa kushirikiana na vyombo vya dola kudhibiti dawa hizo.

Vituo vingine vya habari vilivyotumika kutoa elimu katika mwaka 2022 ni pamoja na TBC 1, ITV, Channel 10, Radio one, Clouds FM, Uhuru FM, Magic FM, Mlimani TV, Kasibante FM, Kagera Community Radio, Radio Rumuli, Radio Mbiu, Dodoma FM, Newala FM, Highland FM, Mashujaa FM Pamoja na Kiss FM. Vile vile, Mamlaka imeandaa Jarida linaloitwa "*Dawa za Kulevya".* Jarida hili linalotoa habari kuhusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kusambazwa kwa jamii ili kuongeza uelewa juu ya masuala ya dawa hizo.

**iv Majukwaa ya kitaaluma**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilipata fursa ya kutoa elimu kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Makatibu Muhtasi, Wakaguzi wa Ndani wa Mahesabu na Wafamasia.

**V. Vyombo vya Ulinzi na Usalama**

Mamlaka katika kuhakikisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinapata elimu sahihi itakayo waongezea ujuzi wa udhibiti wa dawa za kulevya ilifanya uelimishaji kwa maafisa 67 wa Majeshi kutoka nchi 16 za Afrika kwenye Chuo cha Ukamanda JWTZ, Duluti -Arusha; Maafisa 100 wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC); Maafisa wanafunzi wa TAKUKURU wapatao 600 kwenye shule ya Polisi Moshi, Mkoani Kilimanjaro; Makuruta wapatao 600 wa Jeshi la Uhamiaji pamoja na viongozi wao kwenye kambi ya Boma Kichakamiba wilayani Mkinga, mkoani Tanga; Makuruta wa Jeshi la Zimamoto wapatao 397 pamoja na viongozi wao kwenye kambi ya Chogo, wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga na Walimu wa Chama cha Skauti na viongozi wengine wa skauti waliofikia 60, jijini Tanga.

Mamlaka pia ilifanya uhamasishaji wa mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa Kamati za Ulinzi na Usalama pamoja na viongozi wa kijamii wa Mikoa ya Arusha, Mbeya na Mwanza ambapo takribani watu 400 walinufaika na elimu hiyo. Mamlaka ilitoa elimu kuhusu Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Maafisa Upepelezi wa Jeshi la Polisi wanaoshughulikia mashauri ya dawa za kulevya mkoani Tanga.

**vi. Asasi za Kiraia**

Washiriki 91 kutoka Asasi za kiraia zinazowahudumia waraibu wa dawa za kulevya walipata elimu juu ya mabadiliko mbalimbali yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya ya Mwaka 2015.

**vii. Viongozi wa Dini**

Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa Kamati ya Taifa ya Amani na Maridhiano inayohusisha viongozi wa dini mbalimbali. Lengo ni kufikisha elimu ya dawa za kulevya kwa waumini kwenye mahubiri yao.

**viii. Maadhimisho ya Kitaifa**

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau ilitumia Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Dawa za Kulevya Duniani ambayo kitaifa ilifanyika mkoani Dar es salaam kutoa elimu na kuikumbusha jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya.

Aidha, Mamlaka ilishiriki katika maadhimisho mbalimbali ya kitaifa kutoa elimu ya dawa za kulevya kama vile Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) mkoani Dar es salaam, Maonesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane) mkoani Mbeya, Maadhimisho ya Wiki ya Vijana yaliyoambatana na Kilele cha Mbio za Mwenge na Siku ya Kumbukizi ya Kifo cha Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere mkoani Kagera na Maadhimisho ya Wiki ya UKIMWI Duniani mkoani Lindi. Katika maonesho hayo wananchi kutoka mikoa husika na jirani walipata elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya na wengine walipata kupitia vyombo vya habari.

**ix. Wadau wanaojihusisha na kemikali**

Wasimamizi wa kemikali, wasafirishaji, watumiaji, wajasiriamali na walimu wa sekondari wa somo la Kemia wapatao 1,669 kutoka mikoa ya Dar es alaam, Mwanza na Dodoma walipewa elimu kuhusu udhibiti wa kemikali bashirifu na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na.5 ya Mwaka 2015.

### 4.4.2 Uelimishaji uliofanywa na Asasi za Kiraia

Wadau mbalimbali hushiriki kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ili kuhakikisha jamii kubwa zaidi inafikiwa na elimu hiyo. Serikali kupitia Mamlaka huratibu na kuwezesha utekelezaji wa jitihada hizo. Mwaka 2022, Asasi za kiraia 61 zilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa wanufaika 2,258,345 katika taasisi za elimu, waraibu wa dawa za kulevya na jamii kwa ujumla kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 4.1: Asasi zilizotoa Elimu ya Dawa za Kulevya Mwaka 2022**

| Na. | Jina la Asasi | Mkoa | Idadi ya Waliofikiwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanafunzi | Jamii | Waraibu |
| 1. | Antialcoholism and Drug Addiction Organization (AADAO) | Dar es Salaam | - | 206 | - |
| 2. | Blue Cross Tanzania | Arusha | 3,139 | 1,720 | - |
| 3. | Changamoto ni Matumaini | Dar es Salaam | 230 | 390 | 80 |
| 4. | Community Peers for Health and Environment Organization (CPHEO) | Dar es Salaam | 150 | 1,084 | 889 |
| 5. | Drug Abuse | Dar es Salaam | 3,800 | 2,070 | - |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Prevention Organization (DAPO) | | | | |
| 7. | Gift of Hope Foundation | Tanga | - | 3,063 | 227 |
| 8. | Green Hope | Tanga | 192 | 2,000 | - |
| 9. | Guluka Kwalala | Dar es Salaam | - | - | 20 |
| 10. | Harakati Network Organization | Dar es Salaam | - | 958 | 17 |
| 11. | International Organization of Good Templars (T-IOGT) | Dar es Salaam | 86,681 | 2,367 | - |
| 12. | Juza Waste Pickers Initiative | Dar es Salaam | - | - | 149 |
| 13. | Kibao Salama Foundation | Dar es Salaam | - | 82 | - |
| 14. | Kibao Salama Foundation | Pwani | - | 77 | - |
| 15. | Kibwena Community Development | Dar es Salaam | - | 4,815 | - |
| 16. | Kimara Peer Educators and Health Promoters Trust Fund | Dar es Salaam | - | - | 3,110 |
| 17. | Kimara Peer Educators and Health Promoters Trust Fund | Arusha | - | - | 893 |
| 18. | Kiona Youth Coordinates | Tanga | - | 170 | - |
| | | Dar es Salaam | - | 2,000,000 | - |
| | | Zanzibar | - | 260 | - |
| 19. | Kirumba Movement for Harm Reduction | Dar es Salaam | - | 6,921 | 16 |
| 20. | Kusini Culture | Dar es Salaam | 1,500 | 1,850 | 600 |
| 21. | Life and Hope Rehabilitation Organization | Dar es Salaam | 300 | 368 | 450 |
| | | Pwani | - | - | 241 |
| 22. | Lindi Support Agency for Welfare (LISAWE) | Lindi | - | 263 | - |
| 23. | Mama's & Papa's for | Pwani | 36 | - | - |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Community Reform (MPFCR) | | | | |
| 24. | Matumaini Group | Dar es Salaam | 57 | 1,922 | 45 |
| 25. | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) | Dar es Salaam | 2,200 | 86 | 432 |
| 26. | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) | Dodoma | 1,300 | - | 317 |
| 27. | Mtwara Non-Governmental Organization Network | Mtwara | - | 523 | - |
| 28. | Mtwara Society Against Poverty (MSOAPO) | Mtwara | - | 392 | - |
| 29. | Mapambano ya Kifua Kikuu na UKIMWI Temeke (MUKIKUTE) | Dar es Salaam | - | - | 955 |
| 30. | Nazareti Kwaya | Dar es Salaam | - | 400 | - |
| | | Iringa | - | 350 | - |
| | | Tanga | - | 320 | - |
| 31. | Next Generation Keepers | Dar es Salaam | 700 | 5,120 | - |
| 32. | Ngao Youth Group | Dar es Salaam | 138 | 34 | - |
| 33. | Nugget Development Tanzania | Dar es Salaam | 6,096 | 15,00 | - |
| 34. | Organization of Youth Against Risk Behaviours (OYARB) | Dar es Salaam | 800 | 1,210 | - |
| 35. | People with Drug Dependence and Relief Foundation (PEDDEREF) | Ruvuma | - | 690 | - |
| 36. | Peer to Peer Supporting Group | Dar es Salaam | - | - | 364 |
| 37. | Rafiki wa Watoto (RAWATO) | Mwanza | 607 | 83 | 31 |
| 38. | Recovery Brotherhood | Iringa | 220 | 600 | 18 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 39. | Recovery Youth with Vision (REYOVI) | Dodoma | 10,000 | 20,000 | 500 |
| 40. | Saikolojia Sensitization Networking of Tanzania (Saiko Senta) | Dodoma | 263 | 981 | 15 |
| 41. | Serve Tanzania (SETA) | Mbeya | - | 74 | 51 |
| 42. | Social And Economic Support for Drug Abuse Free Environment (SESDE) | Dar es Salaam | 100 | - | - |
| 43. | Steps Tanzania | Dar es Salaam | 351 | 12 | 363 |
| 44. | Tandika Youth and Handcraft Group (TAYOHAG) | Dar es Salaam | - | - | 335 |
| 45. | Tanzania Network of People Who Use Drugs (TANPUD) | Dar es Salaam | - | - | 262 |
| 46. | Tanzania Albinism Society | Dar es Salaam | - | 300 | - |
| 47. | Tanzania Community Empowerment Organization (TACEO) | Pwani | 260 | 180 | - |
| 48. | Temeke Combating Illicit Drugs Organization (TECIDO) | Dar es Salaam | 718 | 31 | 749 |
| 49. | The Helper Organization | Mbeya | 120 | 60 | 148 |
| 50. | Tanzania Organization of Good Templars (T-OGT) | Dar es Salaam | 5,187 | 342 | - |
| 51. | Volunteers for Youth in Health and Development | Mtwara | - | 150 | - |
| 52. | Waungwana Group | Dar es Salam | 4,900 | 16,791, | 110 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kagera | | 578 | |
| 53. | Women Support Group | Dar es Salaam | - | - | 100 |
| 54. | Wounded Healers Organization | Mbeya | - | 80 | - |
| 55. | Youth Achievement Village in Tanzania (YAVT) | Dar es Salaam | 1,600 | 17,450 | - |
| 56. | Youth and Community Rehabilitation (YCR) | Bagamoyo | 550 | - | 3,175 |
| | | Arusha | 300 | - | 3,110 |
| | | Dodoma | 910 | - | 2,000 |
| | | Dar es Salaam | 60 | - | 2,345 |
| 57. | Youth Community Capacity Enhancement (YOCOCE) | Dar es Salaam | - | 414 | - |
| 58. | Youth Counselling and Rehabilitation Center (YCRC) | Dar es Salaam | - | 227 | - |
| 59. | Youth Empowerment and Psychotherapy Aid Organization (YEPAO) | Kilimanjaro | 2,385 | 1,130 | - |
| 60. | Youth Empowerment Society Tanzania (YES Tanzania) | Kilimanjaro | 420 | - | - |
| 61. | Youth Volunteers Against Risk Behaviours (YOVARIBE) | Dar es Salaam | - | 150 | 599 |
| | | **Jumla** | **136,270** | **2,099,359** | **22,716** |
| | | **Jumla Kuu** | **2,258,345** | | |

# SURA YA TANO
# KUPUNGUZA MADHARA YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

## 5.1 Utangulizi

Matumizi ya dawa za kulevya yanaambatana na madhara ya kiafya kama vile maambukizi ya VVU, homa ya ini, kifua kikuu pamoja na magonjwa ya akili. Sura hii imejikita katika kuelezea utekelezaji wa nguzo ya kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya katika mwaka 2022.

## 5.2 Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu

Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupunguza madhara kwa kutoa tiba, huduma za utengamao na elimu ya upunguzaji madhara kwa waraibu wa dawa za kulevya. Jitihada zilizofanyika ni pamoja na kupanua na kuimarisha huduma za tiba katika vitengo mbalimbali vya afya ya akili, tiba saidizi kwa waraibu kwa kutumia dawa (Medically Assisted Therapy -MAT), nyumba za upataji nafuu na huduma za unasihi. Aidha, mafunzo ya stadi za kazi yamekuwa yakifanyika kwa waraibu wa dawa za kulevya ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea na kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Pia, Mamlaka imekuwa ikiandaa miongozo mbalimbali ya kuratibu uanzishwaji na uendeshwaji wa vituo vya kutolea huduma ya methadone, usimamizi wa nyumba za upataji nafuu, uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya, asasi za kiraia na vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

### 5.2.1 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya Katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini

Katika kupunguza madhara ya dawa za kulevya serikali imeendelea kuboresha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya katika vitengo vya afya ya akili vilivyopo katika hospitali za wilaya, mikoa na rufaa nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2022, jumla ya waraibu 854,134, wanaume wakiwa 434,847 na wanawake 419,287 walipatiwa huduma ya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya kama vile bangi, mirungi, heroin, cocaine na vilevi aina ya pombe na sigara katika vitengo hivyo.

Baadhi ya waraibu walibainika kutumia dawa za hospitali zenye asili ya kulevya kama vile Valium, Pethidine na Tramadol, hali iliyosababishwa na kukosekana na kupanda kwa bei ya dawa za kulevya mitaani pamoja na kuimarika kwa udhibiti wa dawa hizo.

**Jedwali Na. 5.1: Idadi ya Waraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini Mwaka 2022**

| Na. | Jina la Kituo | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwananyamala RRH | 39,176 | 47,342 | 86,518 |
| 2 | Temeke RRH | 31,564 | 37,180 | 68,744 |
| 3 | Bombo RRH | 19,462 | 13,546 | 33,008 |
| 4 | Mount Meru RRH | 18,079 | 10,349 | 28,428 |
| 5 | Amana RRH | 23,585 | 33,974 | 57,559 |
| 6 | Morogoro | 17,010 | 13,022 | 30,032 |
| 7 | Mawenzi | 9,980 | 12,585 | 22,565 |
| 8 | Maweni | 11,337 | 16,549 | 27,886 |
| 9 | Musoma | 16,956 | 7,999 | 24,955 |
| 10 | Sekou Toure | 27,859 | 19,671 | 47,530 |
| 11 | Bukoba | 26,811 | 14,474 | 41,285 |
| 12 | Shinyanga | 13,460 | 14,569 | 28,029 |
| 13 | Geita | 11,768 | 9,258 | 21,026 |
| 14 | Manyara | 8,793 | 10,781 | 19,574 |
| 15 | Tumbi | 24,612 | 32,036 | 56,648 |
| 16 | Dodoma | 17,869 | 9,878 | 27,747 |
| 17 | Singida | 8,778 | 4,382 | 13,160 |
| 18 | Tabora | 7,759 | 5,879 | 13,638 |
| 19 | Katavi | 9,806 | 8,984 | 18,790 |
| 20 | Rukwa | 5,670 | 8,953 | 14,623 |
| 21 | Njombe | 7,862 | 7,843 | 15,705 |
| 22 | Iringa | 13,412 | 12,387 | 25,799 |
| 23 | Mbeya | 19,073 | 16,586 | 35,659 |
| 24 | Ruvuma | 8,996 | 9,078 | 18,074 |
| 25 | Simiyu | 9,788 | 11,240 | 21,028 |
| 26 | Mtwara | 9,970 | 12,890 | 22,860 |
| 27 | Lindi | 6,444 | 7,965 | 14,409 |
| 28 | Songwe | 8,968 | 9,887 | 18,855 |
| | **Jumla** | **434,847** | **419,287** | **854,134** |

### 5.5.2 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya (Medically Assisted Therapy - MAT)

Matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya jamii ya afyuni kama vile heroin, pethidine na tramadol hutolewa katika vituo maalumu vya kutolea tiba kwa waraibu kwa kutumia dawa na huduma za unasihi (MAT) katika kuwasaidia kuondokana na uraibu wa dawa hizo. Dawa zinazotumika kutibu uraibu katika vituo hivyo nchini kwa sasa ni Methadone na Buprenorphine. Aidha, vituo hivi hutoa tiba za magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile magonjwa ya akili,

UKIMWI, kifua kikuu, magonjwa ya ngono na homa ya ini. Huduma nyingine zinazotolewa ni pamoja na uzazi wa mpango, tiba kwa watoto waliozaliwa na tatizo la uraibu kutoka kwa mama zao, tatizo la udumavu pamoja na magonjwa ya kinywa, ngozi, vidonda na majipu.

Utaratibu wa utoaji huduma huanza kwa asasi za kiraia kuwaibua na kuwaandaa waraibu katika ngazi ya jamii ambapo waraibu hupata elimu sahihi na huduma ya unasihi kabla ya kufikishwa katika vituo vya MAT. Asasi hizo ni MEFADA, YCR, YOVARIBE, MUKIKUTE, KISAFO, OTARB, Gift of Hope Foundation, SETA, IRDO, Peer to Peer na Kimara Peers. Hadi kufikia mwezi Desemba 2022, waraibu wapatao 13,696, wanaume 13,089 na wanawake 607 walipatiwa matibabu katika vituo 15 vya MAT nchini. Vituo hivyo vinapatikana katika mikoa ya Dar es Salaam (7), Pwani (2), Mbeya (1), Songwe (1), Mwanza (1), Dodoma (1), Arusha (1) na Tanga (1) kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 5.2: Idadi ya Waraibu waliosajiliwa kwenye Huduma za MAT hadi kufikia Desemba 2022**

| Na. | Jina la Kituo | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili | 3,284 | 126 | 3,410 |
| **2.** | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala | 3,086 | 242 | 3,328 |
| **3.** | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke | 2,666 | 97 | 2,763 |
| **4.** | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya | 417 | 18 | 435 |
| **5.** | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Sekou Toure-Mwanza | 619 | 23 | 642 |
| **6.** | Kituo cha Itega jijini Dodoma | 544 | 19 | 563 |
| **7.** | Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, Pwani | 513 | 8 | 521 |
| **8.** | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tumbi, Pwani | 360 | 4 | 364 |
| **9.** | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Bombo, Tanga | 683 | 19 | 702 |
| **10.** | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mount Meru - Arusha | 469 | 33 | 502 |
| **11.** | Kituo cha Afya Tunduma mkoani Songwe | 125 | 3 | 128 |
| **12.** | Kituo cha Segerea, Dar es Salaam | 102 | 5 | 107 |
| **13.** | Kituo cha Mbagala -Round Table, Dar es Salaam | 150 | 6 | 156 |
| **14.** | Kituo cha Vijibweni-Kigamboni, Dar es Salaam | 11 | 0 | 11 |
| **15.** | Kituo cha Tegeta, Dar es Salaam | 60 | 4 | 64 |
| | | **13,089** | **607** | **13,696** |

### 5.2.3 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)

Nyumba za upataji nafuu ni nyumba ambazo waraibu wa dawa za kulevya na vilevi vingine hutunzwa na kupatiwa huduma kwa kupitia hatua kumi na mbili (12) za upataji nafuu na unasihi ili kuwaondoa katika utegemezi wa dawa za kulevya. Mamlaka imeendelea kusimamia uanzishwaji, uendeshaji na kuratibu shughuli zinazofanyika katika nyumba za upataji nafuu kwa kuzingatia mwongozo wa uanzishwaji na uendeshaji wa nyumba hizo.

Hadi kufikia Desemba 2022, Jumla ya waraibu 3,180 kati yao wanaume 3,056 na 124 wakiwa wanawake walipatiwa huduma za tiba na utengamao katika nyumba za upataji nafuu. Nyumba hizo zinapatikana katika mikoa 10 nchini kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na.5.3: Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu Mwaka 2022**


| Na | Mkoa | Jina la Nyumba | Waraibu waliopata huduma | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Jumla |
| 1. | Dar es Salaam | Arise and Shine Sober House | 34 | - | 34 |
| | | Changamoto ni Matumaini | 80 | - | 80 |
| | | Drug Abuse Prevention Organization (DAPO) | 56 | - | 56 |
| | | Drug Free Tanzania – The Right Way Recovery House | 63 | - | 63 |
| | | Drug Free Tanzania – The Ties That Bind Us Recovery Center | 34 | - | 34 |
| | | Pillimissanah Foundation (Wanaume) | 225 | - | 225 |
| | | Pillimissanah Foundation (Wanawake) | - | 35 | 35 |
| | | The Awaited Rehab Centre | 25 | - | 25 |
| | | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (1) | 123 | - | 123 |
| | | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (2) | 96 | - | 96 |
| | | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (3) | 21 | - | 21 |
| | | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (4) | 53 | - | 53 |
| | | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (5) | 76 | - | 76 |
| | | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (Wanawake) | - | 42 | 42 |
| | | Kipepeo Foundation – South Beach Sober House | 35 | - | 35 |
| | | New Vision of Life Society Sober House (Second Chance for Addicts) | 36 | - | 36 |
| | | Hope Again Rehabilitation and Wellness Foundation | 33 | - | 33 |
| 2. | Arusha | Foundation for Wellness and | 71 | - | 71 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Youth Tutelage (Olmotonyi Recovery House) | | | |
| | | Northern Hill Sober House | 28 | - | 28 |
| | | Surrender for Freedom Treatment Centre | 97 | - | 97 |
| | | Tanzania New Future Rehabilitation Organization (TAFRO) | 41 | - | 41 |
| | | Tanzania Sobriety and Rehabilitation Organization (Arusha Recovery Sober House) | 105 | - | 105 |
| | | Tanzania Sobriety Change Foundation (Meru Recovery Sober House) | 95 | - | 95 |
| | | Tanzania Sobriety Change Foundation (Njiro Recovery Sober House) | 100 | - | 100 |
| | | Tanzania Sobriety Change Foundation (Usa River Recovery Sober House) | 80 | - | 80 |
| | | TASOR Sober House | 47 | - | 47 |
| **3.** | Kilimanjaro | Kilimanjaro Community Recovery Organization | 68 | - | 68 |
| | | Kilimanjaro New Vision and Sobriety | 121 | 19 | 140 |
| | | Serenity Gate Rehab (SGR) | 7 | - | 7 |
| | | Kilimanjaro Recovery Home (Goodwill and Inspiration for Youth Vision Organization (GIYVO) | 170 | - | 170 |
| | | Surrender for Freedom Treatment Centre | 70 | - | 70 |
| **4.** | Pwani | Life and Hope Rehabilitation Organization | 460 | 6 | 466 |
| | | Mamaz and Papaz Sober house | 21 | - | 21 |
| | | The Light of Miracle Organization 0 Women's Hope Rehabilitation | - | 22 | 22 |
| | | New Vision of Life Socity Sober House | 85 | - | 85 |
| **5.** | Tanga | Courage on Recovery Foundation | 84 | - | 84 |
| | | Gift of Hope Foundation | 40 | - | 40 |
| | | Tanga Drug Free Organization | 49 | - | 49 |
| **6.** | Iringa | Iringa Sober House | 63 | - | 63 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **7.** | Morogoro | Kipepeo Foundation – Free at Last Sober House | 64 | - | 64 |
| **8.** | Dodoma | MRC Tanzania Kigamboni Sober House (7) | 9 | - | 9 |
| **9.** | Mwanza | Pillimissanah Foundation | 65 | - | 65 |
| **10.** | Kagera | Sobriety Forever Rehabilitation Centre | 26 | - | 26 |
| | | **Jumla** | **3,056** | **124** | **3,180** |

**Jedwali Na. 5.4: Idadi ya Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu kuanzia mwaka 2019 hadi Mwaka 2022**

| Mwaka | | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi** | **Me** | 3,609 | 2,103 | 2,949 | 3,161 | **11,822** |
| | **Ke** | 74 | 74 | 160 | 124 | **432** |
| **Jumla** | | **3,683** | **2,177** | **3,109** | **3,285** | **12,254** |
| | | | | | | |




**Kielelezo Na. 5.1: Idadi ya Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu kuanzia mwaka 2019 hadi Mwaka 2022**

### 5.3 Huduma ya Upunguzaji wa Madhara ya Uchangiaji wa Mabomba ya Sindano kwa Wajidunga

Upunguzaji wa madhara kwa waraibu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga hutolewa katika asasi maalumu za kiraia kwa waraibu kwa kutumia dawa na huduma za kuzuia uchangiaji wa mabomba ya sindano (NSP) katika kuwasaidia wajidunga kuondokana na uhatarishi wa kupata maambukizi ya magonjwa

yanayoweza kuambukizwa kwa njia ya damu kama vile UKIMWI, Homa ya Ini aina ya B na C na magonjwa ya ngono. Aidha, Asasi hizo hutoa pia elimu kuhusu tiba za magonjwa mengine yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya yakiwemo ya akili, kifua kikuu, magonjwa ya ngono na magonjwa yasiyoambukiza. Huduma nyingine zinazotolewa ni pamoja na huduma ya usafi pamoja, unasihi pamoja na rufaa ya magonjwa mbalimbali kwa waraibu.

Asasi hizo ni MUKIKUTE, MEFADA, YCR, YOVARIBE, KISAFO, OYARB, Gift of Hope Peer to Peer na Kimara Peers. Hadi kufikia mwezi Desemba 2022, waraibu 3,150, walipatiwa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

### 5.4 Umuhimu wa Huduma za Upunguzaji madhara kwa Waraibu

Huduma za upunguzaji madhara kwa waraibu zina umuhimu kwa waraibu na jamii kama ifuatavyo: -

i. Kutibu uraibu na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya;

ii. Kupata fursa ya huduma mtambuka kwa waraibu ikiwemo tiba ya magonjwa yanayoweza kuambatana na utumiaji wa dawa za kulevya kama vile maambukizi ya VVU, kifua kikuu, homa ya ini na magonjwa ya zinaa;

iii. Kupunguza vifo vitokanavyo na kuzidisha kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya;

iv. Kuwarudisha waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya katika shughuli za uzalishaji na hivyo kuwaondoa katika hali ya utegemezi;

v. Kupunguza matendo ya uhalifu na uvunjifu wa Amani;

vi. Kuondoa unyanyapaa kwa wathirika wa dawa za kulevya katika jamii;

vii. Kuongezeka ufuasi mzuri wa dawa za kufubaza makali ya VVU na kutibu kifua Kikuu hivyo kuondoa uwezekano wa kupata usugu wa dawa hizo miongoni mwa waraibu; na

viii. Kupunguza idadi ya waraibu wa dawa za kulevya hivyo kupunguza soko la dawa hizo

### 5.5 Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka katika mwaka 2022

Mamlaka ina jukumu la kuratibu na kusaidia shughuli zinazofanywa na asasi na vikundi mbali mbali vya kijamii vinavyoshiriki katika kupiga vita dawa za kulevya Nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo Mamlaka iliziwezesha asasi tano (5) kufanikisha jitihada zao katika kutoa elimu na tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya. Asasi hizo zimeainishwa kwenye jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 5.5: Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka mwaka 2022**

| Na. | Jina la Asasi | Mkoa |
|---|---|---|
| **1.** | Waungwana Family | Dar es Salaam |
| **2.** | Free at Last Sober House | Morogoro |
| **3.** | Sobriety Forever Rehabilitation Centre | Kagera |
| **4.** | Changamoto ni Matumaini | Dar es Salaam |
| **5.** | The Light of Miracle Organization - Women's Hope Rehabilitation | Pwani |

# SURA YA SITA
# USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA

## 6.1 Utangulizi

Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka ambalo linahitaji jitihada za pamoja kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa kama moja ya nguzo ya kupambana na tatizo hilo. Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya imeendelea kutekeleza mikakati ya nguzo hii kwa kuendeleza ushirikiano na wadau.

## 6.2 Ushirikiano wa Kitaifa.

Katika kipindi cha mwaka 2022, Mamlaka imeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, Wizara zenye dhamana ya Afya, Elimu, Mambo ya Ndani, Mambo ya Nje, TAMISEMI, Sheria, Fedha, Kilimo, Maendeleo ya Jamii na Usafirishaji katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Taasisi zilizoshirikiana na Mamlaka ni pamoja na Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA), Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Idara ya Usalama wa Taifa, Jeshi la Uhamiaji, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Anga, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Baraza la Famasia.

Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeendelea kushirikiana na Asasi zisizo za kiserikali katika kuzuia uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waraibu. Baadhi ya Asasi zilizoshirikiana na Mamlaka zimeanishwa katika sura ya nne na tano.

Katika kuongeza wigo wa kudhibiti uchepushaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali bashirifu Mamlaka ikishirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Bohari ya Dawa (MSD) na Baraza la Famasia imeendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa kampuni binafsi zinazojihusisha na kemikali na dawa tiba kushiriki katika udhibiti kupitia mradi wa Public Private Partnership (PPP). Hadi kufikia Disemba 2022 kampuni 43 zilisaini mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa mradi huo.

## 6.3 Ushirikiano wa Kimataifa

Ushirikiano umeendelea katika ngazi ya kimataifa kwa kufanya kazi ya mapambano ya dawa za kulevya kwa ukaribu na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) lenye makao makuu Vienna, Austria.

Nchi yetu imeendelea kutekeleza Mkataba wa Makosa ya Jinai yanayovuka mipaka (Transnational Organized Crime- TOC) wa mwaka 2000 unaozungumzia uhalifu wa kupangwa ambapo tatizo la dawa za kulevya lilizungumziwa.




**Kielelezo Na. 6.1: Wajumbe kutoka Tanzania wakiwa kwenye Mkutano wa Kamisheni ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani (CND) jijini Vienna, Austria.**

Serikali imekuwa ikishirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa katika kupambana na kudhibiti tatizo la dawa za kulevya kwenye maeneo makubwa matatu ya kimkakati ambayo ni ukamataji, utoaji wa elimu, tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya. Baadhi ya wadau wakubwa kwa upande mashirikiano hayo katika upande wa ukamataji wa wauzaji na wasambazaji wa dawa za kulevya na kemikali bashirifu ni pamoja na Drug Enforcement Adminstration (DEA) ya Marekani, Ubalozi wa India, National Crime Agency (NCA) ya Uingereza, Naval Criminal Investigative Services (NCIS) ya Marekani, Combined Maritime Force ya Canada, Royal Canadian Mounted Police-CANADA (RCMP), EU-ACT, Indian Ocean Forum on Maritime Crime na International Narcotic Control Board (INCB).

Kutokana na ushirikano huo, Mamlaka imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuzuia uingizaji wa dawa za kulevya kupitia baharini pamoja na kwenda kufanya upekuzi wa baadhi ya meli katika bahari kuu kulingana na Sheria za Kimataifa. Ushirikiano huu umewezesha kubadilishana taarifa za kiintelijensia na kufanikisha kuharibu mitandao mikubwa ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Wadau wa maendeleo kama vile PEPFAR-CDC, Global Fund (GF) na EU-ACT wamekua mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya upunguzaji uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya. Aidha taasisi hizi kwa kushirikiana

na Mamlaka zimeweza kuratibu mafunzo kwa watoa huduma za afya kwa waraibu wa dawa za kulevya.

### 6.4 Ushirikiano wa Kikanda

Nchi yetu kwa kupitia Mamlaka imekuwa ikishiriki katika Mkutano wa kila mwaka wa Viongozi wa Vyombo vinavyopambana na dawa za kulevya Afrika ujulikanao kama HONLEA Afrika. Lengo la mkutano huo wa kila mwaka ni kubadilishana uzoefu, kushirikiana katika upatikanaji wa taarifa pamoja na kupanga mikakati ya pamoja katika udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya barani Afrika. Nchi yetu ilishiriki pia katika mkutano wa mwaka 2022 wa HONLEA ambao ulifanyika Nairobi Kenya.

Tanzania iliingia mkataba na nchi ya Msumbiji na Afrika Kusini (Trilateral Planning Cell-TPC) katika kufuatilia wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya. Mkataba huo unahusisha kubadilishana taarifa za kiintelijensia zinazohusu dawa za kulevya na uhalifu wa kupanga (Transnational Organized Crime) na kujengeana uwezo katika mapambano ya dawa za kulevya. Kwa mwaka 2022, maafisa nane (8) kutoka Tanzania walishiriki katika mafunzo ya upekuzi na ukamataji yaliyoendeshwa na Trilateral Planning Cell chini ya uratibu wa UNODC yaliyofanyika Cape Town, Afrika Kusini.

# SURA YA SABA
# CHANGAMOTO NA MIKAKATI

## 7.1 Utangulizi

Sura hii imeainisha changamoto na mikakati katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya Nchini.

## 7.2 Changamoto

Zifuatazo ni changamoto zinazokabili udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini: -

i. Mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia inayotumika katika biashara ya dawa za kulevya;

ii. Uelewa mdogo wa jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya;

iii. Unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevya hurudisha nyuma jitihada za matibabu;

iv. Kuibuka kwa dawa mpya za kulevya (NPS) na kemikali bashirifu ambazo hazipo katika Sheria za Udhibiti wa Kimataifa;

v. Ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi husababisha udhibiti wa dawa za kulevya kuwa mgumu;

vi. Kukosekana kwa shughuli za kufanya kwa waraibu wanaopata nafuu, hivyo kujikuta wanarudia matumizi ya dawa za kulevya.

vii. Kukosa vifaa au vitendea kazi vya kisasa ambavyo vinaweza kutumika katika kukabiliana na mbinu mpya wanazozitumia wahalifu wa dawa za kulevya katika kusafirisha dawa hizo.

viii. Uhaba wa rasilimali watu na rasilimali fedha.

## 7.3 Mikakati

Mipango ya baadaye katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya ni kama ifuatavyo: -

i. Kuendelea kuboresha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura 95) ya mwaka 2015 kulingana na mahitaji ya wakati huo;

ii. Kupanua huduma za tiba kwa waaraibu wa dawa za kulevya;

iii. Kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki katika utoaji elimu na udhibiti wa upatikanaji wa dawa za kulevya ndani na nje ya nchi; na

iv. Kuimarisha ushirikiano na mamlaka za udhibiti pamoja na wadau wote kwa ujumla.